# Sheria zitumike kuepusha mifugo kuvamia mashamba

**DAR ES SALAAM**

NA THEONESTINA KAIZA-**BOSHE**

Wafugaji kuachia mifugo yao kuvamia mashamba ya wakulima limekuwa tatizo la muda mrefu, hivyo kuonekana kutokuwa na tiba na badala yake linaendelea kukua na kutandawaa sehemu nyingi zaidi nchini kila kukicha.

Kibaya zaidi ni kwamba uvamizi huo unazidi kubadilika taswira, badala ya kuwa ni matukio ya bahati mbaya, au uzembe, sasa unakuwa wa makusudi na wahusika kudiriki kutoa sababu ya kufanya hivyo kwamba ni kukosa malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao.

Kama hiyo haitoshi, imefikia wachungaji wa ng'ombe kulazimisha wakulima waache mifugo yao ile mazao mashambani mwao. Hii peke yake ni ukatili usio na kifani. Na ole wao wakatae kuruhusu mifugo kula mazao mashambani mwao!

Kipigo kitakachotembezwa hapo, wakulima wanajikuta wanasalimu amri. Hadi hatua hii inafikiwa, kunakuwa kuna majeruhi, na hata waliopoteza maisha! Kama ningekuwa ninasoma haya vitabuni, ningeona ni hadithi kama zile za Esopo au za kufikirika.

Sasa sijui tuite ni hadithi ya namna gani inapofikia wafugaji kuwafukuza wakulima kwenye makazi yao ili mifugo yao ile mazao kwa raha na amani bila ukinzani wowote!

Hili limetokea Rufiji na limetangazwa na vyombo vya habari na kuonekana mubashara katika televisheni siku za karibuni. Hili si kwamba limetokea kwa ajali, ama ghafla.

Matukio ya mifugo kuvamia mashamba Rufiji yamekuwapo kwa muda sasa yakiwa yameanza tangu mwaka 2007 mifugo ilipohamishiwa pwani na kusini kutoka Ihefu.

Mwanzoni mifugo kuvamia mashamba ilionekana kama uzembe wa wachungaji.

Tangu wakati huo tumekuwa tukipata habari mbalimbali za kusikitisha kuhusu mifugo kuvamia mashamba na Hifadhi ya Selous.

Wakati mmoja nilishuhudia kashi kashi hizo wakati nimekwenda kufanya uchunguzi kwa ajili ya mradi wa uhifadhi Selous Mashariki. Japokuwa wakati ule ilionekana kama uvamizi huo ulisababishwa na uzembe wa wachungaji, watu tulikosa amani.

Siku moja nilishindwa kufanya mahojiano kutokana na vurugu zilizotokana na uvamizi wa ng'ombe. Kwa ujumla imekuwa mazoea likitokea linalohusu mifugo kuvamia mashamba, tunasikia watangazaji wa habari na polisi wakiita matendo hayo kuwa ni migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

Mtindo wa vyombo vya dola na serikali kuchukulia uvamizi wa mashamba kuwa ni migogoro, kunafifisha uzito, ubaya, ama uovu wa matendo hayo.

Si tu kwa kutowachukulia wahusika wa matendo hayo hatua stahiki, bali pia kutokuona na kutokabiliana na madhara ya matukio hayo kijamii, kiuchumi na kimaendeleo.

Hali hii imekuwa hivyo muda mrefu kiasi cha wafugaji kujenga mazoea, na jamii kubaki njia panda.

Utaratibu wa sasa ni kuwapa wavamizi siku kadhaa waondoke, na kukamata mtu mmoja au baadhi kwa kosa la kujeruhi au kuua; wengine wote wanaondoka zao na kuendelea na maisha yao wanavyopenda.

Kwa upande wa wakulima, hali hii imeendelea kuwaumiza na hata wengine kufikia kuachana na kilimo kabisa na kufanya shughuli nyingine.

Kwa mfano, kuna wakulima wengi Bagamoyo walioacha kulima kutokana na kadhia za mazao yao kuliwa na mifugo, walinzi wa mashamba kujeruhiwa, ama kusumbuka na uvamizi wa mara kwa mara.

Vitendo hivyo vimeendelea sehemu za Fukayosi na Kidomole vikiwa na taswira ya uvamizi na ukatili wa wafugaji kwa wakulima.

Katika maeneo hayo, huwezi kuzungumzia uvamizi wa ng'ombe kwenye mashamba ya wakulima kuwa ni mgogoro kati ya wafugaji na wakulima, maana maeneo husika si ya wafugaji.

Wafugaji wanalo eneo lao katika Kijiji cha Fukayosi ambalo kwa sehemu kubwa limeuzwa na kujengwa.

Linaloshangaza na kuwavunja nguvu wakulima ni kwamba maeneo hayo, kama ilivyo maeneo mengine nchini, yana viongozi wa serikali na kisiasa lakini uvamizi huo na maasi yameendelea na kukua bila kuwapo kwa hatua thabiti za kuukomesha. Mbali na kujenga hofu, hali hii inazidi kupandikiza chuki baina ya wahusika na kudumaza maendeleo katika eneo hilo lote kwa ujumla.

Kinachoudhi ni wafugaji kuonekana kama wapo juu ya sheria za nchi. Hivyo kuruhusu hali hii kuendelea, ni kuruhusu jamii kuwa na matabaka mawili ya wananchi; tabaka moja likiwa ni la wafugaji (wachungaji); wanaofanya wanavyotaka na kudharau na kuwaumiza wakulima sasa wanaokuwa tabaka la wananchi walio chini ya sheria, ama tabaka la wanyonge.

Hali hii haitakiwi kuendelea, na inaweza kukomeshwa kwa muda mfupi tu serikali ikidhamiria. Nasema hivi kwa sababu, kwanza kisheria na kijamii haikubaliki.

Pili, inadidimiza uchumi kwa kuathiri uti wa mgongo wa uchumi wa nchi, na kufukarisha tabaka la wananchi walio wengi.

Sababu ya tatu, ni kwamba hali hii inadumaza maendeleo kifikra, kijamii na kiuchumi kwa kuendekeza uchungaji badala ya ufugaji, desturi isiyokuwa na tija na inayohujumu uchumi.

Nne, ni hali inayojenga chuki ya kimatabaka, na inayoendelea kukua kadiri siku zinavyokwenda na kusababisha madhila makubwa kwa jamii ya wakulima, ikiwa ni pamoja na kukosa amani, kufukarika na kuwa na chuki dhidi ya wafugaji.

Hii ni hali isiyotakiwa kuwapo Tanzania kwa kisingizio chochote kile. Kwanza, kuna ardhi tele isiyotumika. Pili, wafugaji wanaweza kutumia mifugo yao kwa kuiuza na kupata fedha za kuchimba visima na malambo ya kunyweshea mifugo na mashamba/malisho ya mifugo yao. Tatu, wafugaji wanaweza kufuga kisasa, wakawa na mifugo michache yenye tija, hii ni pamoja na kuwa na mashamba ya malisho au chakula cha mifugo. Chakula hicho kinaweza kuwa ni zao jingine la biashara, hivyo kutanua vyanzo vya mapato kwa vijana wa wafugaji na wa wakulima.

Nne, na kubwa zaidi, ni kwamba kuharibu mali ya mtu, kujeruhi na kuua ni makosa ya jinai. Hivyo yanatakiwa kuchukuliwa hivyo, na sheria ichukue mkondo wake. Hili likifanyika litakomesha tatizo la mifugo kuvamia mashamba.

Kwa sasa uvamizi mwingi wa mazao unaofanywa na mifugo unachukuliwa kama migogoro baina ya wafugaji na wakulima, jambo linalosababisha hatua za kupambana nao kuwa za usuluhishi wa kisiasa, mathalani, wakuu wa wilaya kuingilia kati na kutoa maagizo ya kisiasa.

Hivyo, badala ya wavamizi kuwajibishwa kisheria, mara nyingi wanapewa muda wa kuondoka kwenye eneo na kuacha wakulima wakipambana na hali zao; huku wakisononeka kwa uchungu wa kupoteza mazao yao.

Wakati mwingine, wao, ama jamaa zao wanakuwa wamejeruhiwa, na pengine wa kupoteza maisha.

Inapotokea mchungaji mmoja au zaidi wakajeruhiwa au kupoteza maisha, kama ilivyotokea huko Kidomole, Bagamoyo.

Miaka ya karibuni, wafugaji watakusanyika kutoka mikoa yote ya jirani wakiwa na silaha zao za jadi na kutaka sheria ichukue mkondo wake.

Inapofikia hapo, hawaridhiki na kazi ya polisi na viongozi wa eneo husika na wilaya; wanataka kuzungumza na viongozi wa ngazi ya kitaifa, hususan wizara inayohusika na mifugo, ama Tamisemi. Katika kisa cha Kidomole, Wamang'ati walikataa kuzika maiti za vijana wawili waliouawa hadi waziri afike kwenye eneo la tukio.

Wakati Wamang'ati wamekusanyika wakisubiri kiongozi wa ngazi ya juu afike eneo la tukio, hali katika maeneo yote ya jirani ilikuwa tete.

Vijana wa Kimang'ati walionekana kila sehemu wakiwa na silaha zao za jadi na wakiwa na mori. Siku hizo mbili na zilizofuata wenye mashamba yaliyovamiwa hawakupata msaada na askari wa eneo hilo walikuwa katika hali ya taharuki, hasa baada ya mmoja wao kuumizwa eneo la Mung'ongo, Fukayosi.

Wakati mwingine wenye mashamba wameshitaki kwa viongozi wa ngazi za chini, na kujikuta wanababaishwa wasipate chochote cha kufidia mazao, ama majeraha! Ikiwa hivyo mara nyingi kunakuwa na mazingira ama hisia za rushwa.

Wakati mwingine viongozi wanahukumu mashauri na kuamuru wafugaji kulipa fidia baada ya uharibifu wa mazao kufanyiwa tathmini na ofisa kilimo, lakini wafugaji wanagomea fidia, au kulipa kidogo. Kibaya zaidi ni wafugaji kutokubali kabisa adhabu, ama kulipa halafu wakalipa kisasi.

Katika kisa kimoja viongozi wa kijiji walimuamuru mfugaji kulipa faini, akalipa lakini baadaye alikwenda kulipa kisasi kwa kufyeka miembe shamba zima. Huyo mkulima tangu shamba lake lifyekwe hajarudi tena kulima.

Kwa mtu yeyote aliyewahi kushuhudia uvamizi wa mashamba na hali inavyokuwa katika kusimamia sheria na kudai haki, atakubaliana na mimi kuwa, kama mashauri haya yataendelea kuchukuliwa na kusuluhishwa kama migogoro, wafugaji wataendelea kutenda matendo ya kikatili na wakulima wataendelea kupata hasara na kuumizwa na chuki itaendelea kukua.

Hivyo kama serikali haitatumia sheria kukomesha ukatili na uvunjaji wa sheria unaofanywa na wafugaji kwa wakulima, itafika mahali yatatokea mauaji makubwa zaidi.

**Mwandishi wa makala hii ni mwanataaluma za Wanyamapori, Mazingira na MaendeleoEndelevu.**
**0762889342**
**tkaiza@gmail.com**



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki.**

ya ombaomba ambayo imekuwa kero

malalamiko katika ngazi za juu ikiwemo

Lueka.

RAIA MWEMA

# Ng'ombe 300,000 kupatiwa chanjo

**Na Lucas Raphael,Tabora**

**HALMASHAURI** ya Wilaya ya Uyui mkoani Tabora inatarajia kutoa chanjo ya ugonjwa wa mapele ya ngozi kwa takribani ngombe 300,000 katika kipindi cha mwezi moja na nusu ujao.

Hayo yamebainishwa juzi na Mkuu wa Wilaya hiyo Kisare Makori alipokuwa akizindua zoezi la chanjo ya mifugo lililofanyika katika kijiji cha Igalula kata ya Igalula wilayani humo.

Alisema lengo la chanjo hiyo ni kulinda mifugo yao isiathiriwe na ugonjwa huo baada ya kubainika mifugo mingi kuathiriwa na ugonjwa huo hivyo kupelekea kushuka kwa mapato na kusababisha hasara.

Makori alisema baada ya serikali kuona changamoto hiyo imeamua kutoa chanjo ili kuua vimelea vya ugonjwa huo ambavyo vimekuwa vikisumbua sana mifugo.

Alifafanua kuwa ugonjwa wa mapele ya ngozi husababishwa na virusi na ng'ombe huambukizwa kwa kuumwa na wadudu kama kupe, mbung'o, ndorobo ikiwemo kuchangia maji, malisho au hewa.

"Ng'ombe akipata maambukizi ya virusi hivyo huota mapele makubwa mwili mzima kwenye ngozi na tumboni na baadaye vipele huumuka na kuwa vidonda," alisema.

DC alibainisha kuwa vidonda hivyo hupenya na kusababaisha magonjwa mengine nyemelezi ambayo huongeza makali ya ugonjwa kwa ng'ombe.

Mkurungezi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya hiyo, Hemed Magaro alitoa wito kwa wafugaji wote kuzingatia maelekezo ya wataalamu wakati wa zoezi la uelimishaji jamii katika vijiji na kata zote ili kudhidbiti ugonjwa huo.

Aidha aliwataka kuchangamkia fursa hiyo punde zoezi hilo litakapofika katika maeneo yao, ili kuepusha athari zaidi kwa mifugo yao huku akiwahakikishia kuwa mifugo itakuwa salama baada ya kuchanjwa.

Awali Afisa Mifugo wa wilaya hiyo Dk Kija Maige alimweleza DC kuwa hadi sasa wameshachanja ng'ombe 81,486 katika kata 16 kati ya kata zote 30 ambapo kila ng'ombe hulipiwa sh 1000.

Alisema mwitikio kwa wafugaji kuleta mifugo yao bado ni mdogo ila wanaendelea kuwahamasisha, ili kuhakikisha kila ng'ombe anachanjwa.

4,000/->> Ni bei ya robota ya malisho ya asili yen

# TALIRI yaagizwa kuongeza uvunaji malisho ya mifugo

Na MWANDISHI WETU

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia mifugo, Tixon Nzunda ameitaka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), kuongeza uvunaji wa malisho ya mifugo katika vituo vyake vyote nchini na kuhakikisha jamii inayowazunguka inajifunza ulimaji wa malisho hayo.

Nzunda alisema hayo mwishoni mwa wiki akiwa katika ziara ya kikazi ya siku moja katika kituo cha TALIRI kilichopo Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma na kutembelea kampasi ya Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA).

Alisema licha ya jamii inayoishi karibu na vituo vya TALIRI kujifunza juu ya ulimaji wa malisho ya mifugo, pia inapaswa kujifunza juu ya teknolojia rahisi ya uvunaji wa malisho na kuelekezwa utaratibu wa ulimaji wa malisho ikiwemo kuandaa mashamba na uvunaji mbegu.

Katibu huyo alishauri sekta binafsi kujikita katika biashara ya malisho ya mifugo kwa kuwekeza katika vifaa vya uvunaji, hususan malisho ya asili ambayo ni biashara yenye faida kubwa, kwani robota moja linauzwa kuanzia sh. 4,000 na kuwekeza katika uzalishaji mbegu za malisho ambazo zinahitajika kwa wingi.

Nzunda aliwataka vijana hususan wasomi, kuchangamkia fursa ya ulimaji wa malisho ya mifugo kwa kupata elimu juu ya ulimaji bora kupitia TALIRI na kuwekeza kulingana na maelekezo watakayopata ili walime kwa faida.

Akizungumza na baadhi ya wafanyakazi wa taasisi ya TALIRI na LITA, aliwataka kufanya kazi kutokana na mabadiliko ya mazingira ya sasa na kuacha mazoea au malalamiko na kutaka kila kitu kitoke katika serikali, badala yake wafanye kazi kutokana na rasilimali inayopatikana kuzidi kuboresha utendaji wa kazi.

Katika ziara hiyo Katibu Mkuu Nzunda, aliambatana na Mwenyekiti wa Bodi ya TALIRI, Profesa Sebastian Chenyambuga, Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo Profesa Erick Komba, Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angello Mwilawa na viongozi wengine.

Katibu huyo pia alikagua ujenzi wa bweni la wanafunzi la LITA na kuutaka uongozi wa kampasi hiyo kuhakikisha jengo hilo linakamilika ifikapo Oktoba, 30, mwaka huu, ili lianze kutumika.

AGIZO

CamScanner

UK16.

## o SUA imefanya utafiti kupata nyasi zinazofaa kwa mifugo

# SUA yazifanyia majaribio nyasi za malisho

**Na WARIOBA IGOMBE,** *Morogoro*

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) cha mkoani hapa, kimeanza kuzifanyia majaribio nyasi za malisho kwa nchi zinazokabiliwa na changamoto ya malisho ya mifugo, ikiwemo Uganda.

Mhadhiri Mwandamizi na Mtafiti wa nyasi za malisho SUA, Dk. Elly Ligate, alisema hayo juzi na kuongeza wameanza kuzifanyia majaribio nyasi hizo nchini Uganda kwa kuwa ni miongini mwa nchi zinazokabiliwa na changamoto ya ukosefu wa majani ya malisho.

"Nchi ya Uganda ni miongoni mwa nchi zinazokabiliwa na changamoto ya ukosefu wa nyasi za malisho, hivyo SUA baada ya kufanya utafiti kwa takriban miaka 20 tumepata nyasi, zinazofaa kwa mifugo nchini humo," alisema.

Dk. Ligate alisisitiza lengo ni kuzifikia nchi nyingi za Afrika zinazokabiliwa na changamoto hiyo na kwamba SUA inafanya kila liwezekanalo kuhakikisha Afrika yote inanufaika na uwepo wake katika sekta ya mifugo.

Alieleza utafiti unaofanywa na wataalamu wa chuo hicho kuhusu utatuzi wa changamoto ya majani ya malisho kwa mifugo kwa nchi za Afrika, umelenga kuimarisha sekta ya mifugo.

Dk. Ligate alisema SUA ni hazina kubwa nchini na Afrika kwa ujumla, kwa kuwa inazalisha wataalamu wa sekta ya mifuko na kilimo.

Mkuu wa Idara ya Sayansi na Viumbe hai wa SUA, Beda Mwang'onde, alisema utafiti uliofanyika miaka kadhaa iliyopita umebaini majani aina ya Juncao ni suluhisho la changamoto ya malisho ya mifugo nchini na maeneo mengine ya Afrika.

Mwang'onde alisema mabadiliko ya tabia nchi yameathiri upatikanaji wa malisho ya mifigo, hivyo majani hayo yameonekana yanafaa zaidi kwa kuwa mbali na kupatikana kwa rahisi, pia ni bora na yananenepesha mifugo.

Balozi wa Uganda nchini, Fred Mwesigye, alieleza kufurahishwa na SUA kwa kufanya utafiti na kuibua teknolojia zenye tija katika sekta ya kilimo na mifugo.